



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO



29/01/2025

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU MIKOPO INAYOTOLEWA KWA
VIKUNDI VYA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAMU.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido anatangaza uwepo wa fedha kwa ajili ya kuvikopesha vikundi vya wanawake vijana na watu wenye ulemamu ambapo jumla ya kiasi cha shilingi 220,000,000 zimetegwa katika robo ya Tatu ya mwaka wa fedha 2024/2025. kuanzia Tarehe 30 Januari 2025 zoezi hilo litaanza rasmi kwa kupokea maombi ya mkopo kwenye mfumo wa wezesha portal.

Aidha mwisho wa kupokea maombi kwa robo ya tatu itakuwa tarehe 10 februari 2025.

Vikundi vinavyotakiwa kuomba mikopo vinapaswa kuwa na sifa zifuatazo:-

- i. Kikundi cha wanawake, vijana na watu wenye ulemamu kilichotambuliwa na kupewa cheti cha utambuzi na halmashauri.
- ii. Kikundi kiwe kinachojishughulisha na shughuli za ujasiriamali mdogo au wa kati au kikundi kinachotarajia kuanzisha shughuli za ujasiriamali.
- iii. Kikundi cha wanawake na vijana kiwe na idadi ya wanakikundi kuanzia watano (5) na kuendelea na kikundi cha watu wenye ulemamu kiwe na wanakikundi wasiopungua wawili (2). Pia kwa kuzingatia kanuni ya 6a (1) mtu mwenye ulemamu anaweza kuwa na sifa ya kupata mkopo kama kikundi cha watu wenye ulemamu endapo timu ya menejimenti ya halmashauri itajiridhisha kuwa amekosa mtu mwingine mwenye ulemamu wa kuungana naye katika eneo lake. Aidha sifa nyingine zitafanana na sifa za vikundi vingine.

- iv. Kikundi kiwe na akaunti ya benki iliyofunguliwa kwa jina la kikundi kwa ajili ya matumizi ya shughuli za kiujasiriamali.
- v. Wanakikundi lazima wawe ni raia wa Tanzania wasio na ajira rasmi, wenye akili timamu na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Aidha, kikundi cha vijana kitapaswa na wanakikundi wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.
- vi. Kikundi kisiwe kinadaiwa mkopo mwingine.

Maombi yote yatumwe kupitia mfumo wa kielektroniki (tembelea tovuti: mikopohalmashauri.tamisemi.go.tz) ili kutambuliwa na kuomba mkopo au wasiliana na afisa maendeleo ya jamii wa kata husika au mtendaji wa kata husika.


Kikundi kinachoomba mkopo kinapaswa kuwa na viambatisho vifuatavyo;

- a) Barua ya kikundi ya kuomba mkopo iliyopitishwa na afisa mtendaji wa kijiji/mtaa.
- b) Muhtasari wa kikundi wa kuomba mkopo.
- c) Andiko rahisi la mradi unaoombewa mkopo kwa kuzingatia fomu iliyo ndani ya mfumo na taarifa ya akaunti ya benki.

Kwa taarifa zaidi tembelea Ofisi za Kata katika eneo lako.

Nakutakia ushirikiano mwema.

Tangazo hili limetolewa na:-



Nassoro B. Shemzigwa,
MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA LONGIDO.